**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**(Jeshi la Magereza)**

# TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, anatangaza nafasi za ajira kwa Vijana wa Kitanzania wenye elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) na wenye ujuzi wa fani mbalimbali kwa ngazi ya Stashahada na Shahada kama zilivyoainishwa katika tangazo hili. Waombaji wote wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:-

1: **SIFA ZA MWOMBAJI:**

a) Awe ni raia wa Tanzania;

b) Awe na Kitambulisho cha Uraia au Namba ya Utaifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA);

c) Awe amehitimu Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au waliopo Makambini;

d) Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini;

e) Awe na umri kati ya miaka 18 - 25 kwa wahitimu wa Kidato cha Nne, na 18 - 30 kwa wenye ujuzi;

f) Awe na Cheti cha Kuzaliwa;

g) Awe na urefu usiopungua futi 5'4" kwa wanawake na futi 5'7" kwa wanaume;

h) Awe na siha na afya njema ya mwili na akili iliyothibitishwa na Daktari wa Serikali;

i) Asiwe ameoa/kuolewa;

j) Asiwe na alama au michoro yoyote katika mwili wake(tattoo);

k) Awe na nidhamu na tabia njema na awe hajawahi kupatikana na hatia kwa shitaka la Jinai Mahakamani na hajawahi kufungwa;

l) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya awali ya Askari Magereza na kufanya kazi mahali popote nchini Tanzania;

m) Awe tayari kujigharamia yeye binafsi katika hatua zote za awali za usaili wa ajira hii hadi kuripoti mafunzoni.

2. **NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:**

I) **Kwa waombaji wa Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV)**

Waombaji wote waandike barua kwa Mkuu wa Gereza lililopo jirani. Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya posta.

Barua za maombi ziambatishwe na nakala zifuatazo:-

a) Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate);
b) Nakala za vyeti vya kuhitimu Kidato cha Nne (Academic Certificate na Leaving Certificate);
c) Cheti cha udhibitisho wa siha njema kutoka kwa Mganga wa Serikali;
d) Nakala ya kitambulisho cha uraia au namba ya utaifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA);
e) Nakala ya Cheti cha kufuzu Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au barua kutoka kwa Mkuu wa Kikosi kwa waliopo Kambini;
f) Picha moja (01) ya *Passport size*;
g) Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa anakoishi mwombaji.

II) **Kwa waombaji wenye ujuzi wa fani mbalimbali:**

Mwombaji anatakiwa kuandika barua yake ya maombi kwa mkono wake (handwriting) na namba yake ya simu ya mkononi inayoweza kupatikana muda wowote. Maombi yao yatumwe kwa Kamishna Jenerali wa Magereza kwa anuani ifuatayo:-

Kamishna Jenerali wa Magereza,
Makao Makuu ya Magereza,
Barabara ya Arusha,
Eneo la Msalato,
S.L.P. 1176,
DODOMA.

Pamoja na barua ya maombi anapaswa kuambatisha nyaraka zifuatazo:-

a) Barua ya utambulisho toka kwa Mtendaji wa Kata au Serikali ya Mitaa/Kijiji anakoishi Mwombaji;
b) Nakala ya Cheti cha Kuzaliwa (Birth Certificate);
c) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au Namba ya Utaifa;
d) Nakala ya Cheti cha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au Barua ya Utambulisho kutoka kwa Mkuu wa Kikosi kwa wale waliopo Makambini;
e) Cheti cha uthibitisho wa siha njema kutoka kwa Mganga wa Serikali;
f) Nakala za vyeti vya Elimu ya Sekondari (Leaving and Academic);
g) Awe na Nakala ya Vyeti vya fani/ujuzi mbalimbali uliotangazwa (Academic certificates and transcripts);
h) Awe na picha moja (01) ya '*passport size*'.

III) **Ujuzi na fani zinazohitajika:**

a) Shahada ya Usimamizi wa Mifumo ya Tehama (Bachelor in Network Administration);
b) Shahada ya Uhandisi wa Programu (Software Engineering);
c) Shahada ya Saikolojia na Ushauri nasaha (Psychologhy and Councelling);
d) Shahada ya Udaktari (Bachelor in Medicine);
e) Shahada ya Uuguzi (Bachelor in Nursing);
f) Shahada ya Famasia (Bachelor in Pharmacy);
g) Shahada ya Afya ya Kinywa (Bachelor in Dental);

h) Shahada ya Upigaji Picha za Mionzi (Bachelor in Radiology);
i) Shahada ya Uhandisi wa Tiba Tendaji (Bachelor in Biomedical Engineer);
j) Stashahada ya Ufundi wa Vifaa vya Ofisi (Diploma of Office Machines);
k) Stashahada ya Utabibu (Diploma in Clinical Medicine);
l) Stashahada ya Uuguzi (Diploma in Nursing);
m) Stashahada ya Famasia (Diploma Nursing in Pharmacy);
n) Stashahada ya Afya ya Kinywa (Diploma in Dental Heath);
o) Stashahada Upigaji Picha za Mionzi (Diploma in Radiology);
p) Stashahada ya Uuguzi wa Viungo (Diploma in Physiotherapy);
q) Stashahada ya Eletroniki na Mawasiliano (Diploma in Electronics and Communications or Electronics and Telecommunications);
r) Stashahada ya Takwimu (Diploma in Statistics);
s) Stashahada ya Kilimo/Mifugo;
t) Stashahada ya Katibu Muhtasi (Diploma in Secretarial);
u) Stashahada ya Lugha za Alama (Diploma in Sign Language).

IV) **Zingatia:**

a) Waombaji wote ambao walishafukuzwa katika kozi za mafunzo ya awali ya uaskari magereza hawaruhusiwi kuomba tena;
b) Barua itayowasilishwa kwa njia ya mkono au barua pepe (email) haitafanyiwa kazi;
c) Mwombaji yoyote atakayewasilisha nyaraka za uongo/kughushi (Forged Documents) atakuwa ametenda kosa la jinai hivyo atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 26 Januari, 2024.

Imetolewa na:-

Mzee R. Nyamka
KAMISHNA JENERALI WA MAGEREZA
09 Januari, 2024